
MWELEKEO WA MSIMU WA MVUA ZA MASIKA (MACHI – MEI, 2022) KWA MAENEO YA KASKAZINI MWA MKOA WA KIGOMA

**Umetolewa: 17/02/2022**

Taarifa hii inatoa mwelekeo wa msimu wa mvua za Masika katika kipindi cha Machi - Mei, 2022; athari na ushauri kwa sekta za kilimo, mifugo na uvuvi katika maeneo ya kaskazini mwa mkoa wa Kigoma na wilaya zake:

(I) Ngazi ya Mkoa




**Kielelezo 1: (a)** Mwelekeo wa msimu wa Masika, 2022 kwa mkoa wa Kigoma. (b) Ramani inayoonesha wastani wa muda mrefu wa mvua za msimu wa Masika katika maeneo ya kaskazini mwa mkoa wa Kigoma. **Angalizo**: Wastani wa muda mrefu (miaka 30) wa mvua za mwezi Machi hadi Mei, mabadiliko ya mvua kati ya mwaka mmoja na mwingine yamezingatiwa.

**Dondoo**

- *Kwa ujumla mvua za wastani hadi juu ya wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya kaskazini mwa mkoa wa Kigoma.*
- *Mvua zinatarajiwa kuanza wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Februari, 2022.*
- *Mvua zinatarajiwa kuisha wiki ya pili ya mwezi Mei, 2022.*
- *Vipindi vya ukavu vya siku kumi (10) au zaidi vinatarajiwa kujitokeza hususan katika mwezi Mei, 2022.*

**Mvua za msimu wa Masika, 2022**


Kwa ujumla mvua zinatarajiwa kuwa za wastani hadi juu ya wastani katika maeneo mengi ya wilaya za kaskazini mwa mkoa wa Kigoma. Mvua zinatarajiwa kuanza kati ya wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Februari, 2022 na kuisha wiki ya pili ya mwezi Mei, 2022.

***Angalizo:***
*Izingatiwe kuwa maeneo mengi yanatarajiwa kupata mvua za wastani hadi juu ya wastani hivyo matukio ya vipindi vya mvua kubwa zinazoambatana na upepo mkali yanatarajiwa kujitokeza.*

(II) Ngazi ya Wilaya

## MWELEKEO WA MSIMU WA MVUA ZA MASIKA (MACHI – MEI, 2022) KWA WILAYA YA KAKONKO
**Umetolewa: 17/02/2022**

Taarifa hii inatoa mwelekeo wa msimu wa mvua za Masika katika kipindi cha Machi hadi Mei, 2022; athari na ushauri kwa sekta za kilimo, mifugo na uvuvi katika wilaya ya Kakonko.




Mwelekeo wa mvua za Masika Machi-Mei, 2022 kwa wilaya ya Kakonko, Kigoma.

### Dondoo muhimu

- *Mvua za wastani hadi juu ya wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya wilaya ya Kakonko.*
- *Mvua zinatarajiwa kuanza kati ya wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Februari, 2022.*
- *Mvua zinatarajiwa kuisha wiki ya pili ya mwezi Mei, 2022.*
- *Hali ya unyevunyevu wa udongo, upatikanaji wa chakula cha samaki, upatikanaji wa maji na malisho vinatarajiwa kuimarika katika maeneo mengi.*
- *Wakulima na wafugaji wanashauriwa kutumia teknolojia ya uvunaji wa maji ya mvua na uhifadhi wa malisho kwa matumizi ya baadae.*

### Mvua za msimu wa Masika, 2022 kwa Wilaya ya Kakonko

**Zitaanza:** Kati ya wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Februari, 2022.

**Zitaisha:** Wiki ya pili ya mwezi Mei, 2022.

**Kiasi cha mvua zinazotarajiwa:** Mvua zinatarajiwa kuwa za wastani hadi juu ya wastani. Kwa kawaida wastani wa mvua katika miezi ya Machi-Mei kwa wilaya ya Kakonko ni kati ya milimita 400 hadi 405.

**Kiwango cha juu cha mvua:** Kinatarajiwa katika mwezi Aprili, 2022.

**Vipindi vya ukavu:** Upo uwezekano wa kutokea vipindi vya ukavu vya siku kumi (10) au zaidi katika msimu huu wa Masika, 2022.

**Ulinganifu:** Mvua zinatarajiwa kuwa za kutosha na zenye mtawanyiko mzuri katika maeneo mengi ukilinganisha na Masika iliyopita.

### Angalizo:

- **Wakulima, wafugaji na wavuvi wanashauriwa kupata ushauri zaidi kutoka kwa maafisa ugani kwa matumizi sahihi ya taarifa za utabiri wa hali ya hewa.**
- **Watumiaji wa taarifa hii wanashauriwa kufuatilia utabiri wa saa 24, siku 10, mwezi pamoja na tahadhari kila zinapotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.**

### Matokeo na ushauri kwa kilimo, mifugo na uvuvi

**Matokeo**

- Kunatarajiwa kuwa na unyevunyevu wa kutosha katika udongo kwa ajili ya kilimo na malisho ya mifugo.
- Kunatarajiwa kuwa na maji ya kutosha kwa ajili ya mifugo na samaki.
- Magonjwa ya ukungu kwa mimea yanayosababishwa na mvua nyingi yanatarajiwa kujitokeza.
- Kutuama kwa maji hasa maeneo ya mabondeni kunatarajiwa.
- Uharibifu wa mazao pamoja na miundombinu ya umwagiliaji na uvuvi kutokana na mvua nyingi unatarajiwa kujitokeza.
- Magonjwa ya mifugo kama vile kuoza kwato na yale yanayotokana na kupe yanatarajiwa kujitokeza.

**Ushauri**

- Wakulima na wafugaji wanashauriwa kuimarisha miundombinu ya umwagiliaji, mifugo na uvuvi.
- Wakulima wanashauriwa kuandaa mazingira mazuri ya uvunaji, usafirishaji na uhifadhi wa mazao wakati wa mvua.
- Wakulima wachukue tahadhari dhidi ya magonjwa ya ukungu na wafugaji kuchanja mifugo dhidi ya magonjwa.




**Taarifa hii Imetolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania**

(II) Ngazi ya Wilaya

## MWELEKEO WA MSIMU WA MVUA ZA MASIKA (MACHI – MEI, 2022) KWA WILAYA YA KIBONDO
**Umetolewa: 17/02/2022**

Taarifa hii inatoa mwelekeo wa msimu wa mvua za Masika katika kipindi cha Machi hadi Mei, 2022; athari na ushauri kwa sekta za kilimo, mifugo na uvuvi katika wilaya ya Kibondo.




Mwelekeo wa mvua za Masika Machi-Mei, 2022 kwa wilaya ya Kibondo, Kigoma.

### Dondoo muhimu

- *Mvua za wastani hadi juu ya wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya wilaya ya Kibondo.*
- *Mvua zinatarajiwa kuanza kati ya wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Februari, 2022.*
- *Mvua zinatarajiwa kuisha wiki ya pili ya mwezi Mei, 2022.*
- *Hali ya unyevunyevu wa udongo, upatikanaji wa chakula cha samaki, upatikanaji wa maji na malisho vinatarajiwa kuimarika katika maeneo mengi.*
- *Wakulima na wafugaji wanashauriwa kutumia teknolojia ya uvunaji wa maji ya mvua na uhifadhi wa malisho kwa matumizi ya baadae.*

### Mvua za msimu wa Masika, 2022 kwa Wilaya ya Kibondo

**Zitaanza:** Kati ya wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Februari, 2022.

**Zitaisha:** Wiki ya pili ya mwezi Mei, 2022.

**Kiasi cha mvua zinazotarajiwa:** Mvua zinatarajiwa kuwa za wastani hadi juu ya wastani. Kwa kawaida wastani wa mvua katika miezi ya Machi-Mei kwa wilaya ya Kibondo ni kati ya milimita 400 hadi 410.

**Kiwango cha juu cha mvua:** Kinatarajiwa katika mwezi Aprili, 2022.

**Vipindi vya ukavu:** Upo uwezekano wa kutokea vipindi vya ukavu vya siku kumi (10) au zaidi katika msimu huu wa Masika, 2022.

**Ulinganifu:** Mvua zinatarajiwa kuwa za kutosha na zenye mtawanyiko mzuri katika maeneo mengi ukilinganisha na Masika iliyopita.

**Angalizo:**

- **Wakulima, wafugaji na wavuvi wanashauriwa kupata ushauri zaidi kutoka kwa maafisa ugani kwa matumizi sahihi ya taarifa za utabiri wa hali ya hewa.**
- **Watumiaji wa taarifa hii wanashauriwa kufuatilia utabiri wa saa 24, siku 10, mwezi pamoja na tahadhari kila zinapotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.**

### Matokeo na ushauri kwa kilimo, mifugo na uvuvi

**Matokeo**

- Kunatarajiwa kuwa na unyevunyevu wa kutosha katika udongo kwa ajili ya kilimo na malisho ya mifugo.
- Kunatarajiwa kuwa na maji ya kutosha kwa ajili ya mifugo na samaki.
- Magonjwa ya ukungu kwa mimea yanayosababishwa na mvua nyingi yanatarajiwa kujitokeza.
- Kutuama kwa maji hasa maeneo ya mabondeni kunatarajiwa.
- Uharibifu wa mazao pamoja na miundombinu ya umwagiliaji na uvuvi kutokana na mvua nyingi unatarajiwa kujitokeza.
- Magonjwa ya mifugo kama vile kuoza kwato na yale yanayotokana na kupe yanatarajiwa kujitokeza.

**Ushauri**

- Wakulima na wafugaji wanashauriwa kuimarisha miundombinu ya umwagiliaji, mifugo na uvuvi.
- Wakulima wanashauriwa kuandaa mazingira mazuri ya uvunaji, usafirishaji na uhifadhi wa mazao wakati wa mvua.
- Wakulima wachukue tahadhari dhidi ya magonjwa ya ukungu na wafugaji kuchanja mifugo dhidi ya magonjwa.